KENYATTA UNIVERSITY

*Transforming Higher Education...Enhancing Lives*

# MWITO WA MAKALA

## KITABU CHA HESHIMA KWA PROF. GEORGE IRERI MBAABU



### UTANGULIZI

Hii ni awamu ya tatu ya mipango ya kumuenzi Prof. Ireri Mbaabu. Kabla ya kustaafu kwake, Profesa alihudumu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa miaka 46. Amesomea katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Chuo Kikuu cha California, Los Angeles (UCLA), Chuo Kikuu cha Howard, Washington D.C.

Profesa Mbaabu anatambulika kwa kuanzisha Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Kenyatta ambayo aliiongoza kama Mwenyekiti wa Idara kwa miaka mingi. Amehudumu katika nyadhifa mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Baadhi ya hizo ni kuwa mwenyekiti wa Kamati ya Kutathmini na Kupandisha Vyeo Wahadhiri, Mkurugenzi Kituo cha Kuhifadhi Viwango, Mkuu wa Shule ya Fani na Sayansi za Jamii, na Kaimu Mkuu wa Shule ya Shahada za Juu.

Katika kazi yake ya kiakademia, amechangia katika uandishi wa kamusi kama vile *Sheng-English Dictionary*, *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, *Kamusi ya Karne ya 21* na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Miongoni mwa vitabu maarufu vya Profesa ni *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili, Language Policy in East Africa, Sarufi ya Kiswahili, New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Development Research and Literature,* na *Kiswahili Lugha ya Taifa.* Kitabu chake cha hivi karibuni ni riwaya iitwayo *Masomoni California.*

Kutokana na mchango mkubwa aliotoa Profesa Mbaabu katika taaluma ya Kiswahili, Afrika Mashariki na kote ulimwenguni, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta imepanga kuchapisha kitabu cha kumuenzi. Kitabu hicho kitakuwa na anwani: ***Historia na Maendeleo ya Kiswahili.*** Makala zinakaribishwa katika mojawapo ya maeneo yaliyotafitiwa na Profesa Mbaabu, ambayo ni:

- Chimbuko na Maenezi ya Kiswahili
- Lahaja za Kiswahili na Usanifishaji wake
- Sera ya Lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki na kwingineko
- Utamaduni wa Waswahili
- Sheng na ‘lugha’ ibuka
- Kiswahili, Elimu na Lugha za Kiasili
- Sarufi ya Kiswahili
- Fasihi ya Kiswahili
- Uchapishaji
- Uhusiano wa Kiswahili na Lugha Nyinginezo

### MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUANDIKA MAKALA

- Iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- Iwe na maneno kati ya 3500 – 6000.
- Makala ipigwe chapa katika programu ya word.
- Mistari itengane kwa kipimo cha nafasi ya 1.5”.
- Makala iwe na ikisiri
- Mwandishi atumie mtindo wa Times New Roman fonti ya 12
- Makala ihaririwe vizuri.
- Tanbihi zitumike ikiwa tu ni lazima.
- Urejeleaji ufanywe kwa kutumia mtindo wa APA Toleo la 8.
- Ukurasa wa kwanza uoneshe anwani ya makala, jina la mwandishi na anwani yake ya baruapepe.

### TAREHE MUHIMU

Ifuatayo ni ratiba ya kuandaa chapisho:

- 25.06.2021 — Kutolewa kwa mwito wa ikisiri
- 31.07.2021 — Makataa ya kupokea ikisiri
- 15.08.2021 — Arifa kuhusu kukubaliwa kwa ikisiri
- 15.11.2021 — Makataa ya kupokea makala
- 30.01.2022 — Kukamilisha uhariri wa makala
- 30.03.2022 — Uchapishaji kukamilika
- Aprili 2022 — Uzinduzi wa kitabu

**Ikisiri isiyozidi maneno 300 itumwe kwa anwani ifuatayo ya baruapepe: kumuenziprofesambaabu@gmail.com**